

HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DKT. ANGELINE MABULA (MB) WAKATI WA UZINDUZI WA MATOKEO YA UTAFITI WA HAKI NA USALAMA WA UMILIKI WA RASILIMALI ARDHI NA MAKAZI TANZANIA MWAKA 2017/18 UKUMBI, JENGO LA LAPF - DODOMA, TANZANIA TAREHE 28 SEPTEMBA, 2018.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu;

Watendaji Wakuu Serikalini mliopo;

Wawakilishi kutoka Taasisi za Umoja wa Mataifa mliopo;

Wawakilishi kutoka “Global Land Alliance” na Washirika wake;

Washirika wa Maendeleo mliopo;

Wawakilishi kutoka Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi;

Waandishi wa Habari;

Ndugu Washiriki mliopo;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Habari za Asubuhi

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana

Napenda kuungana na waliotangulia kuelezea dhana nzima ya kukutana hapa siku hii ya leo ambayo kwangu mimi kama Waziri mwenye dhamana ya kusimamia **Haki na Usalama wa Umiliki wa Rasilimali Ardhi na Makazi ni siku muhimu sana.** Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imedhamiria kwa dhati kuhakikisha haki na usalama wa umiliki rasilimali ardhi unafuata sheria na taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuhakikisha Wananchi Wanyonge wanapata haki zao za msingi za kumiliki ardhi na makazi yao. Hivyo, matokeo ya utafiti wa leo yatatupatia hali halisi ya mtazamo (perception) wa Wananchi kuhusu kushughulikia umiliki wa ardhi nchini.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana

Naomba nitumie fursa hii ya kuungana na Watanzania wenzetu ambao wamepoteza maisha yao kufuatia ajali ya kuzama kwa kivuko cha MV. NYERERE iliyotokea tarehe 20 Septemba mwaka 2018 katika kisiwa cha Ukara, Wilaya ya Ukerewe Mkoa wa Mwanza. Hadi kufikia tarehe 26 Septemba, 2018 Watanzania wapatao 227 wamepoteza maisha yao katika ajali hiyo. Hii ni nguvu kazi kubwa mno kwa Taifa letu ambayo imepotea. **Hivyo, sote kwa umoja wetu tusimame na kukaa kimya kwa dakika moja ili kuwakumbuka na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na kuwapa wepesi wa kupona haraka majeruhi wote walionusurika katika ajali hiyo - AMINA**

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kama mnavyofahamu Tanzania ni Mwanachama wa Umoja wa Mataifa, kwa msingi huo, utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG's) 2030, Tanzania ina jukumu la kujumuika na Nchi nyingine duniani katika kufutilia utekelezaji wa Malengo 17 pamoja na Shabaha 169. Hivyo, kila mdau hana budi kushiriki katika ufuutiliaji wa Mpango huu wa Kimataifa.

Wizara yangu ikishirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na wadau wengine ni kuhakikisha tunapata viashiria vyote vinavyotupatia uhalisia wa *wapi tulikotoka, hali ilivyo kwa sasa* na *wapi tunakwenda na nini matarajio ya baadae*. Takwimu rasmi ambazo ni shirikishi ni masikio na macho ya suala zima la Dira na Dhamira ya Wizara yangu ninayoiongoza.

Katika utekelezaji wa Mpango huu wa Dunia kuna viashiria vinavyohusu Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nimeelezwa kwa leo Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikishirikiana na Wadau wa Maendeleo imekusanya taarifa za kitakwimu kuhusu *Kiashiria Na. 1.4.2 kinachohusu asilimia ya watu wazima wenye haki ya kumiliki ardhi, na ambao wana nyaraka za kisheria za kuthibitisha uhalali wa umiliki huo na wajione* (perceive) *kuwa wanayo haki ya umiliki, kwa jinsia na aina ya umiliki.*

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kama mnavyofahamu, Wizara yangu imeendelea kufanya kazi kwa bidii na ufanisi mkubwa katika Kuratibu na Kusimamia maendeleo ya Sekta ya Ardhi na Makazi kuendana na Sera na Miongozo mbalimbali ya ardhi kama ilivyoainishwa katika Dira ya wizara inayolenga kumfanya kila Mwananchi kuwa na *uhakika wa umiliki wa ardhi, nyumba bora na makazi endelevu* pamoja na Dhamira yake ya kuweka mazingira yanayofaa kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi, nyumba na makazi Nchini.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Katika kuhakikisha tunatekeleza Dira na Dhamira tuliyojiwekea, wizara yangu imeendelea na juhudi za kupambana na vikwazo vinavyojitokeza wakati wa utekelezaji wa sera na miongozo mbalimbali ya ardhi. Kama mnavyofahamu, *ardhi ndiyo rasilimali namba moja katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 inayohamasisha na kuhimiza Taifa kufikia Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025 kupitia uwekezaji wa viwanda nchini*. Ili kufikia azma hii ya Taifa letu, pamoja na majukumu mengine, wizara yangu ina majukumu makubwa ya *kuandaa na kusimamia mipango kabambe ya matumizi bora ya ardhi hususan katika upangaji wa miji na vijiji, upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani zake, utoaji hati miliki zikiwemo hati za kimila, kusajili hati miliki, kuthaminisha mali, kutatua migogoro ya ardhi na nyumba pamoja na kuhamasisha wananchi kuwa na nyumba bora.*

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kama ilivyoelezwa na waliotangulia dhununi la uzinduzi wa taarifa hii ni kupokea matokeo ya utafiti kuhusu maoni ya Wananchi juu ya masuala ya *haki na usalama katika umiliki wa rasilimali ardhi na makazi* uliofanyika baina ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na watafiti kutoka “*Global Land Alliance*”. Utafiti huu ulihusisha sampuli wakilishi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar na ulihusu kupata maoni ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea (watu wazima) kutoka kaya binafsi juu ya haki na usalama wa umiliki wa rasilimali ardhi na makazi kama wataalam wetu watakavyotoa matokeo yake hivi punde.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kabla ya kupokea matokeo ya utafiti huu napenda kipekee nipongeze jitihada binafsi zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha ndoto ya Tanzania ya kuwa Nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Juhudi kama hizi hususan zinazohusu maendeleo ya ardhi na makazi ni pamoja na kuutangaza mkoa wa Dodoma kuwa makao makuu ya Serikali na hatimae Jiji, na kupandisha hadhi ya hati miliki za viwanja vyote vilivyokuwa vimeandaliwa na CDA 21,124 kutoka miaka 33 hadi miaka 99. Hatua hizi kwa ujumla wake zitaendeleza juhudi za Wananchi katika kujiletea maendeleo kwa kuwa uwekezaji wa ndani na nje ya Nchi utaongezeka, kukuza mitaji ya uwekezaji kwa uhakika wa kupata ongezeko la thamani kutokana na kuwa na umiliki salama (tenure right). Matokeo yake ni kukuza Pato la Taifa na kuondoa umaskini kwa Wananchi wa Tanzania. Takwimu za Wizara zinaonyesha hadi kufikia Mei 2018 jumla ya hatimiliki pamoja na nyaraka za kisheria 79,456 zilikuwa zimesajiliwa. (Hati 30,143 Nyaraka nyingine 49,313). Nyaraka 31,779 zimesajiliwa chini ya Sheria ya usajili wa ardhi (Sura 334) na hati 923 za umiliki sehemu ya jengo zimesajiliwa (Sura 416)

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kwa ufupi, matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2016 na 2018 matokeo yalionesha kwamba, watu wazima waliokuwa wanaishi katika makazi yao kwa sasa wanaona (perception) wana uhakika wa kuishi kwenye makazi au kumiliki ardhi yao kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Katika kipindi cha **mwaka 2016** uhakika wao kuendelea kuishi au kumiliki raslimali ardhi na makazi katika Makazi yao waliyo nayo kwa sasa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ilikuwa **asilimia 53 ukilinganisha na asilimia 55 ya mwaka**

2018. Ni dhahiri kuwa ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha takribani miaka mitatu tangu ilipoingia madarakani mtazamo wa Wananchi juu ya uhakika wa umiliki ardhi na makazi wanaoishi umeongezeka na kuendelea kuwa na imani na Serikali kwa jitihada zinazofanyika ndani ya Sekta ya kuhakikisha kila Mwananchi anatumia *fursa ya raslimali ardhi na makazi katika kujiongezea kipato chake*. Haya ni mafanikio makubwa ambayo wizara yangu inaendeleza kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii kumhakikishia Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umma wa watanzania kuwa Wizara yangu itafanya kila jitihada ili matokeo haya ambayo yamepatikana katika utafiti huu yametupa nguvu mpya ya kuongeza kasi ya usimamizi wa rasilimali hii ya Taifa letu. Tutaendelea kufanya vizuri zaidi ili kuboresha maisha ya watanzania kwa ujumla wake.

Ndugu wageni waalikwa, napenda pia niufahamishe Umma huu pamoja na utafiti mzuri uliotuletea matokeo chanya, nina imani baada ya wizara kuanza kutumia mifumo ya kielectronic katika utoaji Huduma za ardhi, kwa mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi (Intergrated Land Management Information System - ILMIS) ni wazi kasi ya kuwawezesha wananchi kumiliki hati itaongezeka kwa kuwa muda wa uandaaji hati utachukua muda mfupi sana na hapatakuwa na udanganyifu au ugawaji kiwanja kimoja kwa watu wawili.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kiashiria kingine ambacho nitapenda kukiongelea ni idadi ya watu wazima wenye **Nyaraka zinazothibitisha uhalali wa kumiliki ardhi na Makazi**. Kitaifa matokeo yanaonesha idadi ya watu wazima wenye nyaraka iliyothibitishwa kisheria na kukubalika imeongezeka kutoka **asilimia 50** mwaka 2016 ukilinganisha na asilimia 59 mwaka 2018.

Matokeo yameendelea kuonesha kuwa **asilimia 34** ya watu wazima **mwaka 2016** walitumia ardhi na makazi yao kwa ajili ya kuongeza kipato au kuzalisha chochote kwa ajili ya kaya zao. Idadi hii ya watu wazima imeendelea kuongezeka na kufikia **asilimia 38 mwaka 2018**. Maana yake ni kwamba watu wazima kwa sasa wana uwezo wa kuwekeza au kuzalisha cho chote katika ardhi na makazi yao katika kuongeza kipato cha mahitaji ya msingi na chakula katika kaya zao. Haya ni baadhi ya matokeo ambayo nitazindua muda sio mrefu.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Pamoja na taarifa nzuri ya watafiti, napenda kukufahamisha umma kuwa kasi ya utoaji hati imeongezeka. Hadi kufikia Septemba 2018 mwaka wa Fedha 2018/2019,kwa mujibu wa taarifa toka katika Kanda zetu nane

- Jumla ya Hati 25,463 zimeandaliwa katika Halmashauri mbalimbali nchini,
- Hati 17,680 zimewasilishwa ofisi za Kanda kwa ajili ya usajili,
- Hati 9739 zimeshakamilika.

Changamoto tunayoipata kama wizara:-

- Takwimu zinaonyesha kuwa, hati nyingine zimeandaliwa kwenye Halmashauri lakini zilizowasilishwa kwenye Ofisi za Kanda husika ni chache. Hii imetokana na kukosekana kwa vifaa vya kuandalia Hati ikiwa ni pamoja na *Crested Paper, Land Form No. 23A na File Covers*.
- Pia kuna hati nyingi zinaonekana kuwasilishwa kwenye ofisi za kanda lakini Hati zilizokamilika ni chache. Hii imesababishwa na kuwepo kwa Hati nyingi ambazo zimewasilishwa kwenye ofisi za Kanda zikiwa na mapungufu mbalimbali na hivyo kupelekea hati hizo kutokamilika kwa wakati.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Haki na usalama na umiliki wa Rasilimali ardhi na makazi unagusa pia wananchi waishio vijijini ambapo kufikia Mei, 2018 jumla ya vipande vya ardhi 96,257 vilikuwa vimepimwa katika vijiji 91. Hati za hakimiliki za kimila 20,583 zimeandaliwa na

Vijiji 20 vimeandaliwa na Mipango ya makazi ambapo Jumla ya viwanja 18,224 vimepimwa kwa ajili yakuandaliwa hati ya hakimiliki ya kimila.

Kwa mwaka 2018/19 Wizara imejipanga kuandaa hati za hakimiliki za kimila 120,000 Mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 30 na mpango kina wa vijiji na kupima viwanja 20,000/= hii yote nikutaka kumuwezesha mwanachi a kawaida kuwa na uhakika na salama ya miliki yake na kuepusha mgogoro isiyo na tija

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda nitoe wito kwa Wananchi wote kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali inayojali wanyonge na hususan wale wanaoishi vijijini. Tutahakikisha wanapata haki zao za msingi za umiliki wa ardhi na makazi. Tunafahamu Watanzania walio wengi na ambao ni maskini wanaishi vijijini na Wizara yangu inadhamana ya kusimamia eneo hili kama Waziri mwenye dhamana nitajitahidi kwa kadri na uwezo wangu na kuendelea kushirikiana na viongozi wenzangu na Wananchi wote kuhakikisha nyaraka rasmi za umiliki ardhi na makazi zinatolewa na kuendelea kukabiliana na changamoto zilizopo Nchini kuhusu migogoro ya ardhi. Niwaombe Wananchi wote mwendelee kuipa wizara yangu ushirikiano wa kutosha.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Nitumie tena fursa hii kuwaomba Wananchi waendelee kutii Sheria na taratibu zilizowekwa za umiliki wa ardhi na makazi. Rai yangu kwa viongozi wenzangu katika wizara kuwa taarifa ya kitakwimu nitakayozindua leo imesheheni viashiria ambayo *vinatuelekeza tulipo* na *tunapotaka kuelekea* kwa mujibu wa Dira na Dhima ya wizara ninaiongoza.

Takwimu hizi tutazifanyia kazi kwa kuwa hii ndio hali halisi tuliyopewa na wenzetu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu wakishirikiana na wadau wa maendeleo. Wao wameshatimiza wajibu wao sisi tufuutilie Sera kwa lengo la kuwaleta Wananchi maendeleo. Wito wangu kwenu mliopo hapa makabrasha mtakayopewa msiyafungie kabatini sote kwa pamoja tuyasome na kuyafanyia kazi inavyopaswa.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Napenda kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa kufanya utafiti huu ambao umetuongezea ari na nguvu mpya ya kufanya kazi ya kusimamia sekta ya ardhi na makazi. Pili, napenda kuwashukuru Wadau wa Maendeleo na Mashirika ya Umoja wa Mataifa hususan *Benki ya Dunia, Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (UN - Habitat), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) na Taasisi ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (ODI)* kwa msaada wa raslimali fedha na utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa utafiti huu. Kwa kipekee niwashukuru wataalam kutoka “*Global Land Alliance* na Washirika wake kwa kuiweka Tanzania kuwa miongozi mwa Nchi tatu duniani kushiriki katika utafiti huu ambao umetupatia kiashiria cha SDG Na. 1.4.2 Nchi nyingine zilizofaidika na utafiti huu ni India na Colombia. *Nawashukuru sana.*

Mwisho niwashukuru viongozi na Wananchi wote walioshiriki katika utafiti huu na kutoa taarifa sahihi kwa kuwa umuhimu wa takwimu za ardhi na makazi ndio msingi wa kupanga maendeleo endelevu ya kukuza uchumi na hatimae kupunguza umaskini nchini Tanzania.

Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;

Baada ya kusema hayo, napenda kutamka rasmi kuwa niko tayari **KUZINDUA MATOKEO YA UTAFITI WA HAKI NA USALAMA WA UMILIKI WA RASILIMALI ARDHI NA MAKAZI TANZANIA MWAKA 2017/18.**

Ahsanteni sana kwa Kunisikiliza.